**102/1 INSHA MWONGOZO**

1. Mwanafunzi aeleze unyakuzi wa:
   - a) Misitu
   - b) Shule
   - c) Vituo vya polisi
   - d) Mashamba ya watu binafsi
   - e) Makaburi
   - f) Masoko
   - g) Hifadhi za barabara
   - h) Viwanja vya umma
   - i) Hifadhi za maji k.m mito
   - j) Mbuga za wanyama n.k

TANBIHI

- Sura ya tahariri itokeze waziwazi
- Akikosa sura aondolewe maki 4 baada ya kukadiriwa
- Zingatia pande zote mbili za tahariri yaani afafanue hoja na atoe mapendekezo
- Akizingatia sehemu moja tu insha yake ikadiriwe kwa kiwango cha nusu

2. Hii ni insha ya maelezo. Baadhi ya hoja za kuzingatia ni:
   - a) Mwanafunzi kukosa kupokea alama
   - b) Kukosa vyeti
   - c) Kulazimishwa kurudia darasa
   - d) Kukosa shule ya kurudia mitihani yenyewe
   - e) Kupigwa faini
   - f) Kupoteza muda mwingi akiwa nje
   - g) Kutengwa na jamii
   - h) Kuingizwa katika orodha ya wahalifu
   - i) Mustakabali wake kuharibika atakapokuwa akitafuta kazi

j) Kupoteza hela anaporudia darasa/ mitihani

3. Hii ni insha ya methali. Mwanafunzi aandike kisa kinachoafiki methali yenyewe

- Sehemu mbili zijitokeze waziwazi yaani kuvunjika mguu malishoni na kujikokota
- Atunge kisa kinachoonyesha kuumia/kuathiriwa vibaya mtu akiwa mbali na nyumbani/alikotoka. Kisa pia kionyeshe hali ya mtu kutaka kurudi nyumbani/atakapopokelewa lakini anakabiliwa na changamoto ya kutatua jinsi atakavyorejea (kujkokota)
- Dhana ya majuto yaweza kuwepo katika kisa
-

4. Mwanafunzi akamilishe insha kwa maneno yayo hayo

- **Maudhui**
  - Majuto
  - Kunusurika

ADHABU

1. Atumie nafsi ya kwanza katika umoja au wingi
2. Asipotumia nafsi ya kwanza amejitungia swali( maki 01-02)
3. Asipokamilisha insha yake kwa maneno yayo hayo amejitungia swali

TANBIHI

UREFU---robo (maki 1-2)

Nusu(maki 6-10)

Robo tatu (maki 11-15)

Kamili(maki 16-20)

**102/2 KARATASI YA PILI MWONGOZO**

**UFAHAMU**

a) i) Kuvuruga/ kuharibu hali ya maisha ya watu. ***(alama 1)***

ii) Kuwaua watu ***(alama 1)***

b) i)Ugonjwa uletwao na kula chakula kichafu.Dalili zake ni kuendesha,kuumwa na tumbo na homa kali. ***(alama 1)***

ii) Tibii, ugonjwa wa kukohoa damu ***(alama 1)***

c) Kutokana na kasi yake ya kuua watu ***(alama 1)***

d)- Huambukizwa sana kwa watu walio na miaka kati yawalio na nguvu za kutunza jamii/ watasalia wakongwe na watoto wasioweza kujimudu.

- Umesababisha vifo vingi

- Hospitali na zahanati zimeshindwa kukidhi mahitaji ya wagonjwa.***(hoja 3 x 1 = 3)***

e) - Maradhi haya sasa yamekuwa janga la kitaifa

- Makundi ya kujitolea na mashirika mbalimbali yameundwa ili kuwahudumia wagonjwa

- Wagonjwa wengi pia huishia kutibiwa nyumbani

- Wanasayansi na madaktari wanatafuta tiba ***(Hoja 4 x ½ = 2)***

f) - Tuwe na matumaini kwamba siku moja tiba itapatikana

- Tujikinge kutokana na maradhi haya

- Tuwe na subira kwani subira huvuta heri ***(hoja 3 x 1 = 3)***

g) i) Utaratibu wa utendaji au utekelezaji ***(alama 1)***

ii) Wema /baraka/ fanaka/ ustawi **(*alama 1)***

**Maelezo ya kutuza**

- Makosa ya tahajia – Ondoa nusu 6 yaani ½ x 6

  ili kuwa jumla ya alama 3

- Makosa ya sarufi – Usiondoe zaidi ya nusu ya tuzo kwa kila swali.

**UFUPISHO**

1. a. Zaidi ya wakenya milioni 10 wamo hatarini ya kufa njaa kufuatia uhaba wa chakula.

   b. Asilimia 75 ya wakenya wanategemea kilimo kwa chakula (c) mapato ya kifedha

   (d)Kilimo hutoa karibu robo tatu ya nafasi za kazi kwa wananchi (e) pia kuipa serikali karibu robo ya mapato yake kutokana na mazao ya mauzo katika mataifa mengine

2 a. Serikali inafaa kupunguza ushuru unaotozwa bidhaa za kilimo katika maeneo ya Kusini mwa Sahara

b. kuna haja ya kuwajulisha , (c) kuwahimiza, (d) kuwaelimisha wakulima wa mashamba madogo madogo.

(e) Serikali inafaa kufadhili kilimo, (f) kupunguza gharama za pembejeo za kilimo,(g) kuweka sera zinazodhibiti uuzaji na ununuzi wa vyakula hasa baina ya mataifa,(h) kuongeza sehemu ya bajeti inayotengewa kilimo

**Matumizi ya Lugha**

a) **(i) Ala tuli**

Ala za kutamka hutulia bila kusogeana wakati wa kutamka. Mfano ufizi, meno, kaakaa gumu kuromeo, pua (alama 2)

**(ii) Ala sogezi**

Ala za kutamka husogeana mfano midomo na ulimi (Alama 2)

b) Aliyempiga (Alama 3)

c)

| | | |
|---|---|---|
| | S | |
| KN | | KT |
| N | $\overline{S}$ | T |
| Mkoba | Ambao uliporwa | Umepatikana |

(Alama 4)

d) Kerubo- Nomino ya pekee

Jembe- Nomino ya kawaida (Alama 2)

e) Ngombe amekamuliwa maziwa yote

f) Kishazi tegemezi

Miti iliyokatwa na vibarua jana

Kishazi huru

Miti imebebwa leo asubuhi

g) i. Kutanguliza maelezo ya ziada kuhusu kitu kilichotajwa

Mfano: Juma amekuwa akifanya biashara ya samaki wa aina mbalimbali -- dagaa, kamba, penge, pweza, mkamba na pingusi.

ii. Kutanguliza na kumalizia maelezo ambayo au usemi ambao unaingia katikati ya usemi fulani

Mfano Majambari waliokuwa wamejichimbia kwenye ile handaki - wapatao ishirini na wane - waliuliwa na askari.

iii. Kuonyesha kuwa maneno au usemi fulani unahusishwa na mtu Fulani. Mfano: Majambazi wote wasakwe – Rais.

Zozote mbili (1 x 2)

h)

| | Kutendea | Kutendwa/kutendewa | Kutendeka | Kutendeana |
|---|---|---|---|---|
| Kucha | Chia/Chea | Chiwa /Chewa | chika | Chiana |

i.) Vijitu vile ni vyeusi tititi havionekani gizani.

(j.) “Ruheni, acha tabia ya ulevi,” Kasisi alimwambia

k**. )** Shombo- harufu ya samaki aliyevuliwa

chombo- kifaa cha kufanya kazi, zana za kazi

kifaa cha kutilia kitu

Kitu cha kusafiria

Njia ya mawasiliano

Shirika, idara

l.) I-ZI – Tikiti imenunuliwa

Tikiti zimenunuliwa

LI-YA – Tikiti lilinunuliwa

Matikiti yalinunuliwa

m.) Kwea-shuka/teremka

Alisifiwa-alikashifiwa/ alikemewa

n.) Jamila asipoimba vizuri hatapewa zawadi

o.) Onyesha nomino

Zinazoweza kuundwa kutokwa na vitenzi vifuatavyo

i. Sarifu- Msarifu/usarifu
ii. Sebeha- kisebeho

p.) i. udongo ulikuwa mzuri kulimika kwa urahisi

ii. wakulima walilima vizuri sana

q.) i. Shamirisho kitondo - Mtoto

ii. Shamirisho kipozi - uji

iii. Shamirisho ala - jiko

**ISIMU JAMII**

1. Nadharia inayoiona lugha hii kama lugha ya mseto mchanganyiko wa (waarabu, wahindi, waajemi na wenyenji wa pwani).
   Udhaifu wa nadharia hii unatokana na kuwa inaegenea kwenye kigezo kimoja tu cha msamiati.
   Kigezo cha msamiati pekee hakitoshi kuichunguza lugha.
2. Nadharia ya pili ni ile inayoiona lugha ya Kiswahili kama tokeo la ndoa, biashara ya Afrika Mashariki na Waarabu. Udhaifu wa nadharia ni kuwa unaegenea kwenye kigezo cha msamiati wa Kiarabu.
3. Nadharia ya tatu ni Kiswahili ni lugha ya kibantu
   Nadharia hii inatumia ushahidi wa kiisimu (sayansi ya lugha) na kihistoria. Msamiati mkubwa unaopatikana katika lugha ya Kiswahili una asili ya kibantu.

Lafudhi- ni upekee wa mzungumzaji wa kutamka maneno kutokana na athari za lugha yake ya mama, lugha ambazo zinamzunguka na maumbile katika ala za sauti.

**Rejesta-** Ni vilugha vinavyojitokeza katika jamii kwa sababu tofauti kama vile kikazi, eneo atokalo mtu, urafiki aidha wa karibu sana, umri, tabaka nk.

**102/3 FASIHI** **MWONGOZO**

**SWALI LA LAZIMA: DAMU NYEUSI**

a. Msimulizi Abu anaeleza yaliyojiri maishani mwake aipokuwa akitafuta mchumba wakati familia yake ilikuwa imekumbwa na umasikini. Anaeleza alivyoamua kumwoa Amali, msichana katika kijiji chake. Al 4

b. Msemo – kupata jiko (kupata mke)
- Niliangaza macho (nilitafuta huku na kule) al 2

c. Anawakilisha vijana masikini wakaokabiliana na changamoto ya kuwapata wachumba
Anawakilisha vijana wanaokabiliwa na ukosefu wa ajira
Vijana wanaolazimishwa kujitenga na familia zao ili wajitafutie namna ya kukimu mahitaji yao.
Vijana wanaoijpata katika uhusiano wa kimapenzi yasiyo ya dhati
Vijana wanaotia bidii maishani ili wajiendeleze(4 x1=4)

d. Umaskini
Ukosefu wa kazi
Mapenzi bandia
Wazazi kuingilia ndoa za wanao (Amali na mamake) 3x2=6

e. Mwenye bidii
Mwenye kisari
Mkarimu 2x2=4

**SEHEMU B: KIDAGAA KIMEMWOZEA**

a. Mwalimu Majisifu akiwazia matukio yaliyojiri kule wangwani baada ya kuaibishwa kwenye kikao cha wanafunzi, wahadhiri na wananchi waliokusanyika kumsikiliza katika ukumbi wa Chuo Kikuu cha Mkokotoni( al 4)

b. Nasaba Bora – kuficha stakabadhi halali zamashamba ya watu
Amani – alikuwa mwandishi wa Kidagaa Kimemwozea
Lowela – mamake kitoto uhuru
Nasaba Bora – uhusiano wa kimapenzi na Lowela
Ben Bella – Mpenzi wa mashaka ( 2x2=4)

c. Msomi
Mwizi
Katili
Mwenye majuto
Mlevi
Majivuno (6x2=12)

3 Imani – baada ya kuteseka mikononi mwa askari mwishowe anarejeshewa mali yake na ya nduguze
Amani – kuregeshewa hadhi yake kama mwandishi wa Kidagaa Kimemwozea

D.J – kupona baada ya kuumwa na mbwa
Dora – ndoa yake kupona baada ya Majisifu kubadilika
Zuhura – kupata amani baada ya kuondokewa na Nasaba Bora
Wanasokomoko – kupata amani baada ya viongozi wabaya k.v Nasaba Bora kuondoka
Amani – kupata nafuu baada ya kupigwa na Nasaba Bora
Wanawe Majisifu – kupata mjakazi aliyewajali (Imani) japo kwa muda mfupi, na mwisowe watu kuwakubali
Madhubuti – dhiki ya aibu kutokana na vitendo vya babake lakini hatimaye akakubaliwa na Wanasokomoko
Majisifu – dhiki ya ulevi kuondoka na akaheshimiwa tena 10x2=20

**SEHEMU YA C: Mstahiki Meya.**

4. a). Mnenaji ni Diwani III.Anazungumza na Siki. Wako nyumbani kwa Diwani III wameketi barazani wakiburudika kwa sharubati na asusa. Siki amemtembelea Diwani III ili wazungumze kuhusu hali ilivyo mjini Cheneo maana mjini hakuendeki. Al 4

b) Mambo ya watu kuvurumiwa na askari ilhali wanajaribu kudai haki.

. Askari wamejaa mjini na mji ukawa hauendeki.

-Watu wanaogopa kwenda mjini

-Wafanyakazi wa baraza wamegoma. 4x1=4

c) -Wanacheneo wastahili kuchagua viongozi wanaowajali

- Wanastahili kupigania haki zao.

-wabadilishe katiba yao wapate ya kuwafaa.

-wawaondoe viongozi wabaya. (4x1=4)

d) i) Ni mwenye utu

ii) mwenye busara

iii)Msema ukweli
iv)Mweledi wa mambo
v)Amewajibika
vi)Mtetezi wa haki( 6x1=6)
e) msemo kuchoma moyo-
maana yake ni kusikitisha/kukasirisha 2x1=2

5. Msumari wa moto kwenye kidonda ni msemo unaomaanisha hali mbaya kuwa mbaya zaidi./

a) Hali ya Mamake Dadavuo  ni mbaya ni , ni kama kidonda:

-Ni maskini hawezi pata pesa za kununulia makaa

-Hawezi kununua mafuta taa

-Anakosa chakula mpaka yeye na mwanawe huwa wanakula chakula kilichopimwa mbwa wa Bwana.

**Msumari** unaolekezwa kwenye kidonda chake ni

-kuugua kwa mwanawe.

-ukosefu wa matibabu na dawa za mwanawe kule hospitalini

-Ukaripiwa na Waridi

b) Wafanyakazi wana shida chungu nzima ambazo ni kama kidonda

-Wanalipwa vipeni

-Mshahara hucheleweshwa

-Nyongeza ikija ni ndogo mno

-Watoto wao hufukuzwa shuleni kwa ajili ya karo

-Mazingira ya kufanyia kazi ni mabaya.km kuosha vyoo bila glavu

**Msumari** wa  moto kwenye kidonda hicho ni kwamba:

-Wanapotaka kuongea na Meya anasema diary yake imejaa.

-Wanafurushwa na kupigwa kikatili na askari.

-Wanatishwa kufutwa kazi

-Wengine wanauawa wakati wa vurugu nk.Hali yao imekuwa baya zaidi.

c) Kidonda cha Cheneo ni kwamba

-Haipati matibabu ya kuridhisha zahanatini

-Hawana dawa hospitalini

-ina njaa na watu wanakula mizizi na matunda mwitu

-Watoto wake wanawafia kwa ukosefu wa matibabu

**Msumari** kwa kidonda:

-Meya huchaguliwa mara kadhaa na ukurudi uongozini ,kwa hivyo hali yao haibadiliki haraka.

Viongozi wao –isipokuwa Diwani Kheri hawasaidii kwa lolote, hawamwambii Meya ashughulike maslahi yao kwa hivyo hali inakuwa mbaya zaidi.

Isitoshe viongozi wa dini hawajihusishi na kuukosoa uongozi badala yake wanauombea ule uongozi uendelee kudumu

d) Bajeti ya Cheneo kuwa na naksi ni kidonda kwa hivyo pesa zinapaswa kutumiwa kwa uangalifu sana, jambo ambalo Diwani Kheri anapendekeza.

**Msumari** moto kwenye kidonda hiki ni kuwa

-Pesa zinatumika kwa ufisadi na ubadhirifu mwingi mf.

Madiwani wanadai nyongeza na Meya anashurutisha walipwe.

-Mhubiri aaahidiwa laki moja kila mwezi na kugharamiwa petroli kila juma.

-Meya na familia yake wanaishi maisha ya kifahari km.watoto kusomea ng’ambo, kupeleka familia na marafiki kama Bili katika hoteli za kifahari kama vile Kajifahari.

e) Kupanda kwa gharama ya maisha ni kidonda.

-Kuna umaskini mwingi huko Cheneo

-Watu wa hadhi ya chini wanateseka

Kuelekeza **Msumari** juu ya kidonda ni kwamba

-Watu wa chini ndio wanalipa kodi

-Viongozi wanakataa kulipa kodi

-Viongozi wanataka nyongeza ya mshahara na Meya anaamuru waongezwe.Nayo maisha ya ukata yanaendelea kuumiza wananchi wa kawaida.

f) Zahanatini hakuna dawa ni painkillers tu kama Siki anavyosema.Hiki ni kama kidonda.Kinaelekezewa **msumari** juu yake kwa;

-Wanacheneo kuugua kwa wingi na kuja pale zahanatini kwa wingi kuliko awali.

-Meya hashughuliki kuleta dawa,anadanganya karibuni zingefika.

g)Kidonda kingine cha pale zahanatini ni kuwa

-wagonjwa ni wengi

-hakuna dawa

-hospitali ni chafu

-wagonjwa hawana matumaini

Kidonda hiki kinaelekezwa **msumari** juu kwa

-Waridi kukata tamaa na kujiuzulu

-Anawaacha wagonjwa ambao wanamhitaji zaidi, angaa angewapa matumaini.

**Mengine**

-Ukosefu wa ajira kwa vijana

-Mgomo wa wafanyakazi wa Baraza

Lazima mwanafunzi aeleze jinsi msumari ulivyo juu ya kidonda.

10x2=20

## SEHEMU YA D: USHAIRI

### 6. SHAIRI LA KWANZA (UKARAGUNI)

a. Mtunzi anawaeleza vijana waepukane na matumizi ya mihadarati (dawa za kulevya) kwani yeyote anayezitumia huwa sawa na mtu ambaye hujitia kitanzi, yaani dawa hizi huangamiza( al 2 )

b. Hii ni mbinu ya tabaini. Mbinu hii imetumika kuonyesha kuwa kuna aina mbali mbali za dawa za kulevya ambazo vijana wetu hutumia. ( Al 2 kutaja al 2 maelezo)

c. Yafuatayo ni madhara yaliyotajwa;

-Mlevi huwa anajiingiza katika usherati wa kila aina.- Yeye huambukizwa magonjwa hatari ya zinaa kama kaswende na ukimwi.- Mtumizi huwa hana maana yoyote maishani, ni kama mkia wa mbuzi. -Ikiwa ni mwanafunizi, yeye daima hulala darasani, kwa hivyo, hafuati yafunzwayo. -

-Wengine huingiwa na hamu ya kutaka kula zaidi, huleta hasara.- Mlevi daima hurudisha maendeleo ya nchi nyuma. (4x1=4)

d. Ina maana kuwa, wamegeuka kuwa watu wasio na maana yoyote, hawana faida katika jamii. Ni watu wasiotegemewa kwa vyovyote vile katika jamii. ( Al 3 )
e. Hii ni kwa sababu vina vya kati na mwisho katika kila ubeti wa shairi vimebadilika. Hakuna urari wowote wa vina katika se hemu ya ukwapi na utao wa beti zote.( Al 2)

f.

a) Kuamba- kufahamisha/ ambia/ juza

b) Kitanzi – hatarini

c) Umande – afya/ siha/urazini

d) Shabiki – bingwa/ hodari

e) Tama – mwisho ( 5x1=5)

**7.SHAIRI LA PILI**

a) Mke kupiga mumewe,shida katika ndoa, vita nyumbani Nje
*1 x 2 =2*

b) Tarbia – Mishororo minne

Mathnawi – Vipande viwili kwa kila mshororo

Ukaraguni – Vina vyote vinabadilika ubeti hadi ubeti

Sakarani – Linahusisha bahari zaidi ya moja

*4 x 1 = 4*

c) Ndiyo (1) mshororo wa mwisho unarudiwarudiwa ubeti hadi ubeti (1)

d) - Mishororo minne

- Vipande viwili kwa kila mshororo

- Vina vya kati ni ‘ni’ na vya mwisho ni ‘sa’

- Mizani kumi na sita kwa kila mshororo

*4 x 1 = 4*

e) - Inkisari – ‘mebaki badala ya ‘umebaki’

- ‘metanda badala ya ‘limetanda’

- ‘kipokea badala ya ‘ukipokea’

- Mazida – ‘usinifichani’ badala ya ‘usinifiche’

- Kuboronga sarufi – ‘u kamili mume’ – badala ya ‘u mume kamili’

- Utohozi – Wikendi – weekend – mwisho wa juma

- Divosi – Divorce – Talaka 4x1=4

f) i) Ukanipiku – ukanishinda

ii) Nira – kifaa kinachofungwa juu ya shingo la mnyama wa kufanya kazi

iii) Aushi – maisha

iv) Posa – Ujumbe wa ndoa upelekwao na mume kwa mke anayetaka kumuoa

*4x 1 =4*

**Fasihi Simulizi**

8 (a) i) Utanzu- Ushairi simulizi

Kipera- Pembezi

ii) Sifa za pembezi

-huwasifu watu fulani pekee.

- hughanwa/hukaririwa

- huwa imepigwa chuku (2x2)

iii) Umuhimu wa kipera hiki katika jamii.

-hutumiwa kama burudani

- husifu watu fulani pekee

-hufahamisha jamii kuhusu matendo mazuri ya mtu fulani

-hutumiwa kuwahimiza watu fulani waendelee kutenda matendo ya kishujaa.

(4x1)=4

b) i) Maghani ni ushairi ambao hutolewa kwa kalima yaani hukaririwa badala ya kuimbwa.

Mighani ni hadithi za kimapokeo zinazohusu mashujaa au majagina.

ii) Ulumbi ni uhodari wa kutumia lugha kwa ufundi wa kipekee.

Soga ni hadithi fupi za utani au ucheshi.

iii) Mawaidha ni mazungumzo ambayo hutolewa ili kumpa mtu ushauri au nasaha kuhusu jambo fulani.

Mazungumzo ni maelezo ya mdomo kwa lugha ya kawaida kuhusu suala lolote.

iv) Misimu ni semi za muda ambazo hubuniwa na kutumiwa katika mazingira maalum na katika kipindi maalum cha wakati.

v) Lakabu ni jina la msimbo au jina la kupanga ambalo mtu hujibandika ama hubandikwa kutokana na sifa zake za kimaumbile, kitabaka,kitabia au kimatendo.

Malumbano ya utani ni majibizano kati ya watu wawili au makundi mawili ya watu kwa nia ya kutaniana.

@al.2x5=10